JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

Mji wa Serikali - Mtumba, Barabara ya Afya, S. L. P 573 - 40478 Dodoma.
Simu Na: 255(026)2963341/2963346, Nukushi: 255(026)2963348
Barua Pepe: ps@jamii.go.tz, Tovuti: www.jamii.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

MAADHIMISHO YA SIKU YA KIMATAIFA YA HAKI ZA MTOTO YATAKAYOFANYIKA TAREHE 20 NOVEMBA, 2026

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaungana na Mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Haki za Mtoto, ambayo huadhimishwa tarehe 20 Novemba kila mwaka. Maadhimisho hayo yanalenga kujenga uelewa, kutetea na kuimarisha utekelezaji wa haki za mtoto bila ubaguzi. Kihistoaria, tarehe 20 Novemba ndiyo siku ambayo Umoja wa Mataifa ulipitisha Azimio la Haki za Mtoto la mwaka 1959 na baadaye Mkataba wa Haki za Mtoto wa mwaka 1989, ambao Tanzania imeuridhia na inaendelea kuutekeleza.

Kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka huu ni ***"My Day, My Rights, My Future"*** ambayo imepewa tafsiri ya ***"Siku Yangu, Haki Zangu, Kesho Yangu"***. Kaulimbiu hii inatukumbusha kuwa mtoto anapaswa kutambuliwa, kusikilizwa na kushirikishwa katika masuala yanayomhusu. Neno *Siku Yangu* linaonesha umuhimu wa kumpa mtoto nafasi na kumtambua katika jamii; *Haki Zangu* linasisitiza kuwa kila mtoto anastahili kupata haki zake za msingi bila ubaguzi; na *Kesho Yangu* linaonesha kuwa mustakabali wa mtoto na Taifa unajengwa kwa kulinda na kutekeleza haki za mtoto leo.

Hivyo, kaulimbiu ya mwaka huu inatoa wito kwa kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa haki za mtoto zinalindwa na kuheshimiwa wakati wote. Haki hizo ni pamoja na haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa, kushiriki na kutobaguliwa, kama zilivyoainishwa katika Mikataba ya Kimataifa na Kikanda; Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008; pamoja na Sheria ya Mtoto, Sura 13. Haki hizo zinapaswa kuonekana katika maisha ya kila siku ya mtoto kupitia upatikanaji wa huduma bora za kijamii, ulinzi dhidi ya ukatili na mazingira salama ya ukuaji na ustawi.

Kwa msingi huo, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuhakikisha kuwa watoto wanapata haki zao na kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuanzisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto zaidi ya 18,000 katika ngazi mbalimbali; Mabaraza ya Watoto

8,427 katika ngazi ya kijiji/mtaa hadi Taifa; Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Watoto 15,158 katika shule za msingi na sekondari; Vikundi vya Malezi na Matunzo ya Watoto 5,499; na Madawati ya Jinsia na Watoto 420 ndani ya Jeshi la Polisi.

Aidha, Serikali imefanikiwa kuimarisha ushiriki wa watoto katika michezo kupitia Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo Shule za Sekondari Tanzania (UMISETA). Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa watoto wenye ulemavu kwa kutoa vifaa saidizi kama vile vifaa vya breli vinavyowawezesha watu wenye ulemavu wa macho (wasioona au wenye uono hafifu) kusoma, kuandika na kupata taarifa kwa njia ya mguso; visaidizi vya kusikia; viti vya magurudumu; pamoja na vikuza maandishi.

Mafanikio hayo yanaonesha dhamira ya Serikali katika kuimarisha mifumo ya ulinzi, malezi na maendeleo ya watoto. Pamoja na mafanikio hayo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, zikiwemo Asasi za Kiraia, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo, wazazi, walezi na jamii kwa ujumla, itaendelea kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayenyimwa haki zake au kuachwa nyuma. Mathalani, tunapokaribia kufunga shule na kuanza kwa likizo, wazazi na walezi wanahimizwa kutekeleza yafuatayo:

1. Kuwapa watoto muda wa kupumzika, kucheza na kushiriki katika shughuli za burudani zinazolingana na umri wao;
2. Kuwashirikisha watoto katika kazi salama za nyumbani zinazowajengea uwajibikaji na uwezo wa kujitegemea;
3. Kutenga muda wa kuzungumza na watoto, kuwasikiliza na kufahamu changamoto, mahitaji na matarajio yao;
4. Kuwafundisha watoto maadili mema, heshima, nidhamu na upendo miongoni mwao na kwa watu wengine;
5. Kuhakikisha kuwa dawa, vifaa vya moto, umeme na vitu vingine hatarishi vinahifadhiwa katika sehemu salama zisizofikiwa na watoto;
6. Kuwaelimisha watoto kuhusu usalama wao wakiwa nyumbani, barabarani na katika jamii, ikiwemo kuepuka maeneo hatarishi na ukaribu na watu wasiowafahamu;
7. Kusimamia matumizi salama ya simu, televisheni, kompyuta na mitandao ya kijamii, kwa kuwaelimisha watoto kuhusu madhara ya maudhui yasiyofaa, udhalilishaji na vishawishi vinavyoweza kutokea mtandaoni; na
8. Kuwafundisha watoto namna ya kutambua viashiria vya ukatili na kutoa taarifa kwa kutumia namba za dharura, ambazo ni **111 au 112** kwa taarifa za uhalifu na **116** kwa taarifa za ukatili dhidi ya watoto.

Kwa upande mwingine, Serikali inaendelea kuimarisha utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo na mikakati inayolenga kulinda haki, ustawi na maendeleo ya mtoto, ikizingatiwa kuwa uwekezaji katika watoto ni uwekezaji katika mustakabali wa Taifa na kwamba watoto wa leo ndio viongozi na nguvu kazi ya Taifa la kesho. Hivyo, kila mmoja wetu ana wajibu wa kuchukua hatua na kutoa taarifa anapoona au kubaini vitendo vinavyohatarisha usalama na haki za mtoto. Hatua hizo zitasaidia kuhakikisha

kuwa kila mtoto analindwa, anapata haki zake na anapata makuzi katika mazingira yanayomwezesha kufikia uwezo wake kamili.

Tuadhimishe Siku ya Kimataifa ya Haki za Mtoto kwa vitendo kwa kuhakikisha kuwa haki za mtoto zinalindwa na kuheshimiwa kila siku. Tuithamini siku yao, tuziheshimu haki zao na tushirikiane nao katika kuijenga kesho yao iliyo bora. Tukumbuke kuwa ***"Siku Yangu, Haki Zangu, Kesho Yangu"*** si kaulimbiu tu, bali ni wito wa kuchukua hatua za kimkakati za kuhakikisha kuwa kila mtoto wa Kitanzania anapata fursa ya kukua, kustawi na kutimiza ndoto zake.



Charles F. Komba
Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM
07 Novemba, 2026